

Aweso ahaidi ushirikiano zaidi baina ya Wizara na Sekta binafsi.

Na Fredy Mshiu- DAWASA

Waziri wa Maji Mh.Jumaa Aweso (Mb) amezitaka delta binafsi kuongeza ushirikiano na Wizara ya Maji ili kuhakikisha bidhaa zinazotengenezwa zinakidhi ubora na viwango ili ziweze kuwahudumia vyema wananchi.

Mheshimiwa Aweso amesema hayo Jijini Dar es salaam wakati wa ziara katika viwanda vya uzalishaji wa mabomba ya Maji vya Simba pipes Industries na Plasco kwa ajili ya kutambua na kukuza fursa za ushirikiano baina ya Wizara pamoja na sekta binafsi.

Akiwa katika kiwanda Cha SIMBA pipe industries ltd Mh.Aweso alikagua utengenezaji wa malighafi za mabomba na kuwataka waongeze bidii katika kutengeneza bidhaa zenye viwango Bora kwa jamii ili miradi ya Maji iweze kukamilika kwa wakati.

"Mjitahidi kuzalisha mabomba imara, yenye viwango na yenye gharama nafuu ili sisi wizara tuweze kufikisha huduma kwa wananchi wa mijini na vijijini "alisema Aweso

"Hatuna sababu ya kucheleweshwa kwa miradi ya maji Nchini, mabomba ya maji yanapatikana na kutengenezwa hapa hapa kwa ubora zaidi. Hivyo watengenezaji ni wakati wenu sasa kuboresha viwango na kuongeza ubora katika kazi mnazotengeneza" alimalizia Mheshimiwa Aweso

Kwa upande wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) Mkurugenzi wake, Mhandisi Clement Kivegalo amesema RUWASA inawategemea sana watengenezaji malighafi hao ili utekelezaji wa Miradi ya Maji Vijijini ikamilike kwa wakati.

Akiongea kwa upande wa DAWASA ambao pia ni wadau muhimu wa malighafi hizo, Mkurugenzi wa Manunuzi kutoka DAWASA, Bi Hellen Lupogo amesema kuwa DAWASA inaendelea kuunga mkono juhudi za viwanda hivyo kwa kununua bidhaa kutoka kwao kwani zinasaidia kuongeza uharaka wa utekelezaji wa miradi ya maji kwa Wananchi.

Waziri Jumaa Aweso yuko kwenye ziara ya siku mbili Mkoani Dar es salaam inayolenga kujenga ushirikiano baina ya sekta binafsi na Wizara ya Maji.